SUZA ilivyojipanga kutekeleza mradi wa HEET katika mageuzi ya elimu

Jesse Mikofu, Mwananchi

Benki ya Dunia imetoa mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 425 sawa na Sh972 bilioni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) hapa nchini.

Mradi huo unatekelezwa kupitia vyuo vikuu 14, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Tume ya Sayansi, Teknolojia (COSTECH) na taasisi tano za Wizara ya Fedha na Mipango.

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni miongoni mwa vyuo vikuu 14 vilivyobahatika kuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huo wa miaka mitano kuanzia sasa na ukitarajiwa kukamilika mwaka 2026.

Makamu Mkuu wa SUZA, Profesa Mohammed Makame Haji anaeleza jinsi chuo hicho ikiwa ni taasisi pekee katika mradi huo kutoka Zanzibar ilivyojipanga kuutekeleza na kuleta mageuzi makubwa ya kielimu.

SUZA kupitia Serikali Kuu kama sehemu ya kuboresha elimu ya juu, mradi ulitakiwa kuanza 2019 lakini haukuanza kutokana na taratibu za uwasilishaji wa andiko mpaka WB kuhidhinisha badala yake ukaanza mwaka 2021.

"Licha ya kuchelewa kidogo kuanza lakini sisi tulianza hatua za maandalizi katika maeneo ambayo tunayafanyia kazi. Tumekamilisha baadhi ya matayarisho yanayohitajika licha ya kuwapo changamoto za kupokea fedha kutokana na taratibu za uingizaji wa fedha hizo kupitia akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya taasisi husika kisha unaomba kupitia wizara ikiridhika unapatiwa." anasema

Anasema kwa SUZA kulikuwa na taratibu za ziada SUZA pekee ikiwa sehemu ya muungano kwa hiyo kule kukawa na wepesi lakini SUZA ilitakiwa iwe na hatua za ndani kwanza kabla ya kuwasilisha kwenye Serikali ya Muungano.

Fedha za awamu ya kwanza zimeingizwa kutoka akaunti ya SUZA BoT na kuingia katika akaunti ya matumizi.

Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya SUZA ni Dola za Marekani 20 milioni (46.8 bilioni) na fedha hizi zimegawiwa katika awamu nne ya matumizi hivyo zitatumiwa kwa malengo yaliyowekwa mpaka kukamilika kwa mradi wote.

Maeneo ambayo mradi umejikita kwa SUZA ni matatu, eneo la kwanza ni kuboresha miundombinu ambapo kutakuwa na ujenzi na hatua za awali za kutengeneza andiko na taratibu za awali kutangaza zabuni zimekamilika.

Kwa sasa SUZA inamalizia utengenezaji wa michoro ili kutangaza kupata wakandarasi wanaokidhi na wenye vigezo kufanya kazi hiyo. Katika ujenzi, maeneo yatakayojengwa ni matatu; hosteli zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1000, wanaume 500 na wanawake 500.

Pia itajengwa Lab complex kwa ajili ya kuingiza vifaa ambavyo vitakuwa vinahitajika kwa matumizi ya baadaye.

Professa Makame anasema kupitia mradi huo, watajenga jengo la utawala ambalo litakidhi mahitaji ya kiutawala ikiwemo afisi, kumbi za mikutano na mambo mengine ambayo yanaunga juhudi za uendeshaji wa shughuli za SUZA.

Upande mwingine wa mradi, utatoa mafunzo kwa wafanyakazi wa ndani na mafunzo hayo yatakuwa katika ngazi mbili; shahada ya pili (uzamili) na uzamivu (PhD).

Katika maeneo yaliyoainishwa ya vipaumbele vya mradi na hayo yamejikita katika masuala ya sayansi na teknolojia eneo ambalo linahusiana na uendeshaji wa shughuli hizo.

"SUZA tumekusudia kufundisha wataalamu 70 kupitia fedha hizo katika ngazi hizo, na masharti ya kufundisha yanahitaji wataalamu hawa waende katika vyuo vinavyotambulika na vyenye heshima kulingana na maeneo ya umahili walionao.

"Kwa hiyo tutatumia vyuo vya ndani vyenye uwezo na vingine vya nje kutengeneza uwezo mzuri wa watendaji hao baada ya kipindi hiki cha mradi kupata fursa kwa kutumia chuo," anasema

Anasema mchakato huo unakwenda vizuri tayari awamu ya kwanza ya wanaokwenda masomoni yameshafanywa na wakati wowote walioomba na kukidhi vigezo wataruhusiwa kwenda kuanza masomo.

Mradi kwa vile umejikita katika vipaumbele mahussi hta wanaoomba wanatakiwa kujikita katika maeneo hayo hayo.

Eneo la tatu, SUZA itaboresha hali ya masomo, kutakuwa na uandikaji wa programu mpya katika ngazi ya shahada na uzamili, kuangalia mahitaji yaliyopo hivi sasa, lengo kuu ni kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

Hivyo, SUZA hasa imeangalia pia katika maeneo makuu ya kiuchumi na kisekta yaliyopo kwa upande wa Zanzibar ikiangazia katika mpango wa sera ya uchumi wa buluu ikilenga kuongeza nguvu ya wataalamu katika eneo hilo.

Kwa hiyo itakuwa katika masuala ya afya, utalii, kilimo na huduma na kwa upana wake yale maeneo yaliyojikita na sayansi kwahiyo hapa tutapata nafasi kupitia mitahala tuliyonayo ili sasa iweze kuandikwa upya kwa kushirikisha wadau mbalimbali na wale ambao ndio waajiri wa wahitimu wa vyuo.

Kupitia mpango huo watawaweza kupata uhalisia wa programu iwe katika mazingira yapi na kumfanya yule anayemaliza chuo aweze kujiajiri au kuajiriwa.

Professa Makame anasema kwa kipindi kirefu kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya wahitimu wa vyuo wanakosa ujuzi katika soko hivyo kulazimika kuwapa mafunzo mapya, mradi huu utaondosha changamoto hizo.

Katika kuboresha masuala ya taaluma pia kuna kipengele cha kuongeza nguvu ya Tehama, mradi huo utatumika kuongeza nguvu kununua vifaa vinavyohitajika na kuweka mifumo ya kuendesha shughuli za chuo na kuongeza nguvu za kitaaluma.

Bila shaka sasa hivi SUZA ipo hatua za mwisho katika kuanza matumizi ya ofisi mtandao hivyo mradi utaongeza nguvu hiyo.

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

Sanduku la Posta 146, Zanzibar- Tanzania

Tovuti: http://www.suza.ac.tz Barua pepe: vc@suza.ac.tz

Kichocheo cha Maendeleo ya Jamii

KUMBUKUMBU YA MIAKA 23 YA KIFO CHA RAIS WA KWANZA WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA HAYATI MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Baraza la Chuo, Menejimenti na Wanajumuiya wote wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar inaungana na watanzania na waafrika kwa ujumla katika maadhimisho ya kumbukumbu za miaka 23 ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Daima ataendelea kukumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa kuikomboa Tanzania na Afrika ambapo mpaka sasa bado maono yake yanaendelea kusihi ya kuitaka Tanzania kuwa nchi yenye umoja, amani na mshikamano. Aidha Chuo kinaahidi kuyaenzi na kutekeleza falsafa zake kivitendo katika kuleta ustawi wa wananchi kijamii na kiuchumi.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinaahidi kuendeleza juhudi za kutimiza wajibu wake wa kuchangia maendeleo ya elimu nchini na kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kupitia utoaji wa elimu bora.

Kwa taarifa zaidi kuhusu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar tembelea tovuti http:// www.suza.ac.tz



Julius Kambarage Nyerere
(1922 - 1999)

http:// www.suza.ac.tz **vc@suza.ac.tz** **Sanduku la Posta 146** **Zanzibar, Tanzania**

CamScanner